# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR




## SHERIA YA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII NAM. 3 YA 2018 KATIKA LUGHA NYEPESI (KWA UPANDE WA CHETI CHA KUZALIWA PAMOJA NA CHETI CHA KIFO)

# YALIYOMO……………………………………………………………………………………i

DIBAJI ........ iii

UTANGULIZI ........ iv

ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA ........ v

1.0 USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR ........ 1

1.1 Nini maana ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamiii Zanzibar? ........ 1

1.2 Ni yepi matukio ya kijamii? ........ 1

1.3 Matukio yanayotokea wapi yanapaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar? ........ 1

1.4 Kuna aina ngapi za usajili wa matukio ya kijamii? ........ 1

2.0 USAJILI WA CHETI CHA KUZALIWA ........ 1

2.1 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa? ........ 1

2.2 Ni nani anatakiwa kutoa taarifa ya kuzaliwa kwa mtoto? ........ 2

2.3 Ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho wa kuzaliwa kwa mtoto? ........ 2

2.4 Je kama mtoto amezaliwa nyumbani au sehemu nyengine yoyote isiyokuwa hospitali, taarifa yake ipelekwe wapi? ........ 2

2.5 Vipi mtoto aliyeokotwa anaweza kupatiwa cheti cha kuzaliwa? ........ 2

2.6 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa kwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa? ........ 2

2.7 Ni zipi taratibu za kurekebisha taarifa katika cheti cha kuzaliwa? ........ 3

2.8 Taratibu gani zinatumika kubadilisha jina la mtoto katika cheti cha kuzaliwa? ........ 3

2.9 Ni zipi athari za kutokusajili kizazi na kutokuwa na cheti cha kuzaliwa? ........ 3

2.10 Nini afanye mtu aliyepoteza cheti cha kuzaliwa? ........ 4

2.11 Ni zipi ada za cheti cha kuzaliwa? ........ 4

2.12 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa? ........ 4

2.13 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa? ........ 5

2.14 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa cheti cha kuzaliwa kukataliwa? ........ 5

2.15 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa cheti cha kuzaliwa? ........ 5

2.16 Ni yepi Makosa katika usajili wa cheti cha kuzaliwa? ........ 5

2.17 Ni zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu? ........ 6

3.0 USAJILI WA TUKIO LA KIFO ........ 7

3.1 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kifo? ........ 7

Zipo aina mbili za kupata Cheti cha kifo ambazo ni: - ........ 7

3.2 Ni nani anatakiwa kutoa taarifa ya tukio la kifo? ........ 7

3.3 Kuna aina ngapi za usajili wa kifo? ........ 7

3.4 Ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka taarifa ya tukio la kifo? ........................................ 7

3.5 Baada ya kupewa uthibitisho wa kifo (kibali cha mazishi) kutoka kwa Sheha au Hospitali, ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho huo ili kupatiwa cheti cha kifo? ...................... 7

3.6 Ni upi utaratibu wa kurekebisha taarifa katika cheti cha kifo? ............................................ 8

3.7 Ni zipi athari za kutokusajili tukio la kifo na kutokuwa na cheti cha kifo? ........................... 8

3.8 Nini afanye mtu aliyepoteza cheti cha kifo? ......................................................................... 8

3.9 Ni zipi ada za cheti cha kifo? ................................................................................................ 8

3.10 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo? ....................... 9

3.11 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo? ............................................ 9

3.12 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa cheti cha kifo kukataliwa? ..................... 9

3.13 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa cheti cha kifo? ........................................................................................................................ 9

3.14 Ni yepi Makosa katika usajili wa cheti cha kifo ............................................................ 10

3.15 Zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu? .................................................. 10

## DIBAJI

Awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, mara tu baada ya kuingia madarakani pamoja na mambo mengine, iliagiza taasisi zake zinazotoa huduma kwa wananchi kutoa huduma zilizo bora na kwa wakati bila kuleta usumbufu kwa wananchi.

Vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahakikisha wananchi wote wanapata haki na fursa sawa bila kubagua kama inavyosisitizwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Uwepo wa misingi ya haki za binaadamu unabainisha kuwa pamoja na mambo mengine, haki ya msingi ya binaadamu baadaa ya kuzaliwa ni kupewa jina na kutambuliwa ili kurahisisha misingi ya upatikanaji wa haki.

Wakala wa Usajili wa Mtukio ya Kijaamii Zanzibar ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa rasmi chini ya Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018 kwa lengo la kusajili matukio ya kijamii yanayotokea Zanzibar. Matukio hayo ni pamoja na kizazi, kifo, ndoa, talaka na utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi.

Lengo la kufanya Sheria hii kuwa katika lugha nyepesi ni kuwasaidia wananchi wakiwemo wasimamizi, watumiaji na mawakala wengine waliomo katika kila Wilaya za Unguja na Pemba ili kuweza kuifahamu zaidi Sheria ya Wakala wa Usaji wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na utekelezaji wake.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa juhudi zao katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata uelewa wa Sheria, Kanuni na Miongozo yake katika kufanikisha suala la usajili wa matukio ya kijamii. Aidha, tunapenda kuwashukuru Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Jumuiya ya Center for Youth Dialogue (CYD) pamoja na Mradi wa Data Driven Advocacy (DDA) kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutayarisha Kitabu cha Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika lugha nyepesi.

Tunatoa wito kwa wananchi wote kukitumia Kitabu hiki kama nyenzo muhimu katika kutambua taratibu za usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar na kusajili matukio hayo kwa wakati.

## UTANGULIZI

Kitabu hiki cha ''Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar katika Lugha Nyepesi; Kizazi na Kifo'' kimetayarishwa ili kuwawezesha wananchi kuelewa kwa urahisi masuala yanayohusu taratibu ambazo mwananchi anapaswa kufuata baada ya kuzaliwa kwa mtoto au anapofariki mtu katika familia au jamii husika. Kitabu hiki kimeweka wajibu kwa kila mtu anayehusika wakati yanapotokea matukio ya kuzaliwa kwa mtoto au anapofariki mtu. Wajibu huu umeelezewa kwa kina na kufafanuliwa kwamba unaweza kuwa kwa mtu wa karibu wa mtoto aliyezaliwa au mtu aliyefariki au kwa mtu mwengine ambaye kwa dhamana yake katika ofisi fulani, atalazimika kufuata taratibu zilizowekwa katika Sheria. Kutokana na namna mambo haya yanavyofahamika, tumeamua kuyaweka katika kijitabu kimoja, masuala ya ''Kizazi'' na masuala ya ''Kifo'' ili yafahamike kwa urahisi na kila mwananchi.

Katika masuala ya Kizazi, kitabu hiki kimefafanua utaratibu na hatua za kuchukuliwa na mzazi wa mtoto anayezaliwa au mtu mwengine pale mtoto anapokuwa kwenye mazingira mengine nje ya wazazi wake, ikiwemo mtoto aliyeokotwa. Kitabu pia kimeeleza utaratibu wa kufuatwa ili mtoto aliyezaliwa apatiwe cheti cha kuzaliwa na taarifa za mtoto huyo kuingizwa katika daftari la usajili wa kizazi. Utaratibu huo unajumuisha uwasilishaji wa taarifa muhimu zinazohitajika ili kusajili kizazi na kupatiwa cheti cha kuzaliwa pamoja na ada inayotakiwa kulipwa. Aidha, kitabu hiki kinafafanua athari zitakazotokea ikiwa mtu atachelewa kufanya usajili wa mtoto aliyezaliwa na hivyo kuonyesha umuhimu wa kusajili kizazi cha mtoto mapema. Kwa ujumla, masuala mbali mbali yanayohitaji kujulikana na wananchi yameelezwa kwa kutumia lugha rahisi katika kitabu hiki na mwananchi anaweza kufahamu kwa wepesi pale atakapokisoma.

Kwa upande wa masuala ya kifo, kitabu hiki kimejaribu kufafanua wajibu wa wananchi kusajili taarifa za kifo pale wanapotokewa na kifo katika jamii zao. Kwa ujumla, kumekuwa na mwamko mdogo wa kusajili na kutafuta vyeti vya vifo pengine kwa kuona kuwa usajili na vyeti hivyo hauna umuhimu mkubwa kwa jamii. Kitabu hiki kinafafanua umuhimu wa kusajili na kupata vyeti vya vifo. Pia, kitabu kimejaribu kubainisha watu wenye wajibu wa kutoa taarifa za kifo pale kinapotokea katika mazingira tofauti, ikiwemo hospitali, nyumbani, kwenye vyombo vya usafiri, katika vyuo vya mafunzo na maeneo mengine mbali mbali. Aidha, athari za kutosajili matukio ya vifo pale yanapotokea zimefafanuliwa katika kitabu hiki. Pamoja na masuala hayo yaliyotajwa hapo juu, masuala mengine mbali mbali yanayohusu usajili wa matukio ya vifo yameelezwa kwa kina ili kusaidia wananchi waelewe kwa urahisi.

Kwa ujumla kitabu hiki kimetayarishwa kwa kuangalia vifungu vya Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2020 na kukiweka katika lugha ambayo inaweza kufahamika kwa urahisi na wananchi. Kwa namna kilivyotayarishwa, kitabu hiki kinaweza kuwa msaada mkubwa kwa jamii katika kujenga ufahamu wa masuala ya vizazi na vifo.

## ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA

- Katiba ya Zanzibar ya 1984
- Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018, pamoja na Kanuni zake (Kanuni za za Usajili wa Matukio ya Kijamii 2020)

## 1.0 USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

### 1.1 Nini maana ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamiii Zanzibar?

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, ni Ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa lengo la kusajili, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa vyeti vya matukio ya kijamii kama vile cheti cha kuzaliwa, cheti cha kifo n.k (kifungu cha 3,4,21,27,35,39,43 Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 1.2 Ni yepi matukio ya kijamii?

Matukio ya kijamii ni:

i. kizazi;
ii. kifo;
iii. ndoa;
iv. talaka;
v. utambulisho wa ukaazi; na
vi. matukio mengine. (kifungu cha 2, Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 1.3 Matukio yanayotokea wapi yanapaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar?

Matukio yanayotokea ndani ya Zanzibar ndio yanayopaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

### 1.4 Kuna aina ngapi za usajili wa matukio ya kijamii?

Zipo aina mbili za usajili wa matukio ya kijamii ambazo ni:

i. Usajili wa matukio ya kijamii ndani ya wakati; na
ii. Usajili wa matukio ya kijamii nje ya wakati.

## 2.0 USAJILI WA CHETI CHA KUZALIWA

### 2.1 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa?

Zipo aina mbili za kupata Cheti cha kuzaliwa ambazo ni: -

- **Ndani ya wakati**

Taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa ndani ya wakati ni kama zifuatazo:

i. kuwa na uthibitisho wa tukio la kizazi (kipande) kutoka kwa Sheha au Hospitali;
ii. kuwasilisha Nakala ya kitambulisho cha mtoa taarifa kinachotambuliwa na Serikali;
iii. kuwasilisha Nakala ya gamba la kliniki la mama mjamzito;
iv. kuwasilisha Nakala ya cheti cha ndoa; au

v. kuwasilisha uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika.

- **Nje ya wakati**

Taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa nje ya wakati ni kama zifuatazo:

i. kuwasilisha barua ya Sheha yenye kuthibitisha kuzaliwa kwa mtoto;
ii. kuwasilisha Nakala ya kitambulisho cha mtoa taarifa kinachotambulika na Serikali;
iii. kuwasilisha Nakala za vitambulisho vya muombaji ikiwa ametimia miaka 18 au zaidi;
iv. kuwasilisha barua ya skuli ya msingi aliyosoma muombaji;
v. kuwasilisha picha mbili za muombaji na mtoa taarifa; au
vi. Kuwasilisha uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika.

## 2.2 Ni nani anatakiwa kutoa taarifa ya kuzaliwa kwa mtoto?

Watu ambao wanatakiwa kutoa taarifa ya kuzaliwa kwa mtoto ni:

i. baba au mama wa mtoto;
ii. mmiliki au msimamizi wa nyumba ambayo mtoto amezaliwa katika mazingira ambayo wazazi wake hawana uwezo wa kutoa taarifa ya kizazi hicho;
iii. mtu mwenye dhamana ya mtoto; au
iv. mtu aliyemuokota mtoto. (kifungu cha 22(1), Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.3 Ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho wa kuzaliwa kwa mtoto?

Sehemu ambayo mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho wa kuzaliwa kwa mtoto ni Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar iliyopo katika Wilaya anayoishi mwananchi.

## 2.4 Je kama mtoto amezaliwa nyumbani au sehemu nyengine yoyote isiyokuwa hospitali, taarifa yake ipelekwe wapi?

Iwapo mtoto amezaliwa nyumbani au sehemu nyengine yoyote isiyokuwa hospitali, taarifa yake inapaswa kupelekwa kwa Sheha wa shehia ambayo mtoto amezaliwa.

## 2.5 Vipi mtoto aliyeokotwa anaweza kupatiwa cheti cha kuzaliwa?

Mtoto alieyeokotwa atapatiwa cheti cha kuzaliwa baada ya Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kupata taarifa kutoka Ustawi wa Jamii. (kifungu cha 24, Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.6 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa kwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa?

Taratibu za kupata cheti cha kuzaliwa cha mtoto wa nje ya ndoa ni kama zifuatazo:

i. kuwasilisha hati za viapo kutoka Mahakamani au Kamishina wa viapo vinavyoonesha ridhaa za wazazi wa mtoto kutumia jina la baba; (kiapo cha Baba kuonesha ameridhia jina lake litumike katika Cheti cha Mtoto, kiapo cha Mama yenye kuonesha ameridhia jina la Baba huyo liweze kutumika jina la Baba huyo katika cheti cha mtoto wake) au
ii. kuwasilisha hati ya kiapo ya mama yenye kuthibitisha jina kamili la mtoto ikiwa hakuna mtu aliyeridhia jina lake litumike kama baba wa mtoto huyo; au
iii. Kuwasilisha barua ya Amri ya Mahkama ikiwa jina kamili la mtoto limetolewa na Mahkama. (Kanuni ya 7 ya Kanuni za Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

### 2.7 Ni zipi taratibu za kurekebisha taarifa katika cheti cha kuzaliwa?

Taratibu za kurekebisha taarifa katika Cheti cha kuzaliwa ni kwamba Muombaji anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, barua hiyo ikiwa imeambatanishwa na: -

i. hati ya kiapo kutoka Mahakamani au Kamishina wa Viapo;
ii. Nakala ya vitambulisho vya muombaji; au
iii. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 40 ya Kanuzi za Wakala wa Usajili wa Matuki ya Kijamii Zanzibar 2020)

### 2.8 Taratibu gani zinatumika kubadilisha jina la mtoto katika cheti cha kuzaliwa?

Iwapo Muombaji anataka kubadilisha jina la mtoto katika Cheti cha kuzaliwa anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ikiwa imeambatanishwa na vielelezo vifuatavyo: -

i. Hati ya kubadilisha jina inayotolewa na Mahkama au Kamishina wa viapo;
ii. Nakala za vitambulisho vya muombaji; au
iii. Uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kifungu cha 25, Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 2.9 Ni zipi athari za kutokusajili kizazi na kutokuwa na cheti cha kuzaliwa?

kutokusajili kizazi na kutokuwa na cheti cha kuzaliwa ni kosa kwa mujibu wa sheria, kosa ambalo linapelekea athari zifuatazo: -

i. kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania Laki mbili na isiyozidi shilingi za kitanzania Laki tano (kifungu cha 53, Sheria Nam. 3 ya 2018);
ii. kukosa kumbukumbu za tukio la kuzaliwa;
iii. kukosa uthibitisho rasmi wa nasaba ya mtoto.
iv. kukosa haki za msingi kama vile kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kitambulisho cha Taifa, Pasipoti, Urithi, Kadi ya bima ya afya n.k.

## 2.10 Nini afanye mtu aliyepoteza cheti cha kuzaliwa?

Mtu aliyepoteza cheti cha kuzaliwa atatakiwa kufika katika Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar akiwa na barua ya Polisi yenye kuthibitisha kupotea kwa cheti husika. (Kanuni ya 46 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

## 2.11 Ni zipi ada za cheti cha kuzaliwa?

Ada za cheti cha kuzaliwa ni kama zifuatazo: (Kanuni ya 6 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

| S/N | CHETI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Cheti cha kuzaliwa cha usajili wa ndani ya wakati (siku 42) na kuombwa ndani ya miezi 3. | TSH. 2,500/= |
| 2. | Cheti cha kuzaliwa cha usajili wa ndani ya wakati (siku 42) na kuombwa baada ya miezi 3. | TSH. 7,000/= |
| 3. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia siku 43 mpaka mwaka mmoja na miezi 11. | TSH. 22,000/= |
| 4. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia miaka 2 – 5 na miezi 11. | TSH. 32,000/= |
| 5. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia miaka 6 na kuendelea. | TSH. 42,000/= |
| 6. | Kubadilisha jina katika cheti cha kuzaliwa. | TSH. 30,000/= |
| 7. | Marekebisho ya herufi katika cheti cha kuzaliwa. | TSH. 20,000/= |
| 8. | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 4,000/= |

## 2.12 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa?

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar italazimika kufuta usajili wa Cheti cha kuzaliwa iwapo: -

i. itabainika taarifa za usajili sio sahihi;
ii. usajili umefanywa kwa njia ya udanganyifu, uongo au rushwa;
iii. cheti cha kuzaliwa kimetolewa kimakosa na kinahitajika kutolewa tena;
iv. usajili wa cheti cha kuzaliwa umefanyika zaidi ya mara moja; au

v. ikiwa kuna Amri ya mahkama ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa. (kifungu cha 49, Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.13 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa?

Usajili wa cheti cha kuzaliwa hufutwa kwa utaratibu ufuatao: -

i. kutolewa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa, taarifa hiyo hutolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na kupewa Muhusika wa cheti kinachotaka kufutwa;
ii. kupewa nafasi ya kujibu taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kuzaliwa kwa muhusika;
iii. kufutwa kwa usajili wa cheti hicho kwa kutolewa notisi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Muhusika; na
iv. kutoa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti hicho katika Gazeti Rasmi la Serikali.

## 2.14 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa cheti cha kuzaliwa kukataliwa?

Ombi la usajili wa cheti cha kuzaliwa linaweza kukataliwa endapo: -

i. taarifa za muombaji sio sahihi;
ii. ombi halikufata utaratibu uliowekwa;
iii. tukio la kuzaliwa halikutokea Zanzibar; au
iv. ombi halikuambatanishwa na vielelezo muhimu vinavyohitajika. (Kifungu cha 21(4), Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.15 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa cheti cha kuzaliwa?

Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, ndani ya Siku 30 atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri anaehusika na usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar. (kifungu cha 21(7), Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.16 Ni yepi Makosa katika usajili wa cheti cha kuzaliwa?

Mambo yafuatayo ni makosa kufanyika wakati wa maombi ya usajili wa cheti cha kuzaliwa: -

i. kutoa taarifa za uongo;
ii. kumtumia mtu mwengine kupata cheti cha kuzaliwa;
iii. kutumia nyaraka zisizo halali;
iv. kumshawishi afisa msajili kufanya usajili kinyume na Sheria;

v. kwa uongo, kudai kupoteza au kuharibika kwa cheti ili kupata cheti chengine;
vi. kurekebisha au kuingiza taarifa kwenye mfumo maalumu kinyume na Sheria;
vii. kuharibu au kujaribu kuharibu cheti cha kuzaliwa;
viii. kunyang’anya au kuchukua cheti cha mtu mwengine;
ix. kutumia cheti cha mtu mwengine;
x. kumiliki cheti zaidi ya kimoja; au
xi. kumruhusu mtu kutumia cheti cha mtu mwengine.

## 2.17 Ni zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu?

Adhabu za makosa yaliotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:

Faini isiyopungua shilingi za kitanzania Milioni moja na isiyozidi shilingi za kitanzania Milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili. (Kifungu cha 53(2), Sheria Nam. 3 ya 2018)

**Mfano wa cheti cha kuzaliwa**

ZANZIBAR GOVERNMENT

**Certified Copy of an entry in a Register of Births**

| Serial No. | Date and Place of Birth | Name (if Any) of Child | Sex | Name of Father | Name of Mother | Residence of Parents (if Separate Residence Both Must be Stated) | Signature, Residence and Qualification of Informant | Date of Registration and Signature of Registering officer | Name if Given after Registration |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

**Certified** to be true copy of the Entry(Reg.No.) of a Birth in the Registrar of Births within the Town District of ………………………………………….Island of Zanzibar

**FEE PAID Tsh……………** Given at the Zanzibar Civil Status Registration Agency, this……….day of …………..20……

Revenue Receipt No………………. of ……………

…………………………………………………

*For* Registrar General of Births and Deaths

## 3.0 USAJILI WA TUKIO LA KIFO

### 3.1 Ni zipi taratibu za kupata cheti cha kifo?

Zipo aina mbili za kupata Cheti cha kifo ambazo ni: -

- **Ndani ya wakati**

  Taratibu za kupata cheti cha kifo ndani ya wakati (ndani ya siku 7 baada ya tukio la kifo) ni kama zifuatazo:

  i. kuwasilisha uthibitisho wa tukio la kifo (kibali cha mazishi) kutoka kwa Sheha au Hospitali;
  ii. kuwasilisha Nakala ya kitambulisho cha mtoa taarifa; na
  iii. kuwasilisha uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 10(1)(a) ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

- **Nje ya wakati**

  Taratibu za kupata cheti cha kifo nje ya wakati (baada ya siku 7) ni kama zifuatazo: -

  i. kuwasilisha barua ya Sheha yenye kuthibitisha tukio la kifo;
  ii. hati ya kiapo cha uthibitisho wa kifo iliyotolewa Mahakamani au Kamishina wa kiapo;
  iii. kuwasilisha Nakala ya kitambulisho cha mtoa taarifa; au
  iv. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 10(1)(b) ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

### 3.2 Ni nani anatakiwa kutoa taarifa ya tukio la kifo?

Taarifa ya tukio la kifo inaweza kutolewa na mtu wa karibu wa marehemu au mtu mwengine yeyote anayefahamu taarifa sahihi za kifo hicho.

### 3.3 Kuna aina ngapi za usajili wa kifo?

Kuna aina mbili za usajili wa kifo ambazo ni usajili wa ndani ya wakati (siku 7) na usajili wa nje ya wakati (zaidi ya siku 7)

### 3.4 Ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka taarifa ya tukio la kifo?

Iwapo tukio la kifo limetokea nyumbani au sehemu nyengine yoyote isiyokuwa hospitali, taarifa yake inapaswa kupelekwa kwa Sheha wa shehia ambayo tukio hilo limetokea.

### 3.5 Baada ya kupewa uthibitisho wa kifo (kibali cha mazishi) kutoka kwa Sheha au Hospitali, ni wapi mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho huo ili kupatiwa cheti cha kifo?

Sehemu ambayo mwananchi anatakiwa kupeleka uthibitisho wa tukio la kifo ni Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar iliyopo katika Wilaya anayoishi muombaji.

### 3.6 Ni upi utaratibu wa kurekebisha taarifa katika cheti cha kifo?

Iwapo mwananchi anahitaji kurekebisha taarifa katika Cheti cha kifo anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ikiwa imeambatanishwa na: -

i. hati ya kiapo kutoka Mahakamani au Kamishina wa viapo;
ii. Nakala ya kitambulisho cha muombaji kinachotambulika na Serikali; na;
iii. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika.

### 3.7 Ni zipi athari za kutokusajili tukio la kifo na kutokuwa na cheti cha kifo?

Kutokusajili kifo na kutokuwa na cheti cha kifo ni kosa kwa mujibu wa sheria, kosa ambalo linapelekea athari zifuatazo: -

i. Kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili na isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano (kifungu cha 53, Sheria Nam. 3 ya 2018);
ii. Kukosa uthibitisho rasmi wa kisheria wa tukio la kifo;
iii. Kukosa haki za msingi kama vile Urithi, Mikopo ya elimu ya juu, n.k.

### 3.8 Nini afanye mtu aliyepoteza cheti cha kifo?

Mtu aliyepoteza cheti cha kifo anatakiwa kufika katika Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar akiwa na barua ya Polisi yenye kuthibitisha kupotea kwa cheti husika. (Kanuni ya 46 ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

### 3.9 Ni zipi ada za cheti cha kifo?

Ada za cheti cha kifo ni kama zifuatazo:(Kanuni ya 11 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

| S/N | **CHETI** | **ADA** |
|---|---|---|
| 1. | Cheti cha kifo cha usajili wa ndani ya wakati (siku 7) na kuombwa ndani ya miezi 3. | TSH. 1,500/= |
| 2. | Cheti cha kifo cha usajili wa ndani ya wakati (siku 7) na kuombwa baada ya miezi 3. | TSH. 3,500/= |
| 3. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kuanzia siku 8 mpaka mwaka mmoja. | TSH. 11,000/= |
| 4. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kaunzia mwaka 1 – 2. | TSH. 20,000/= |
| 5. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kunzia miaka 2 na kuendelea. | TSH. 50,000/= |
| 6. | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 4,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Kurekebisha taarifa katika cheti cha kifo. | TSH. 20,000/= |
| 8. | Kubadilisha jina katika cheti cha kifo. | TSH. 30,000/= |

**3.10 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo?**

Usajili wa cheti cha kifo unaweza kufutwa endapo: -

i. Itabainika taarifa za usajili sio sahihi;
ii. Usajili umefanywa kwa njia ya udanganyifu, uongo au rushwa;
iii. Cheti cha kifo kimetolewa kimakosa na kinahitajika kutolewa tena;
iv. Usajili wa cheti cha kifo umefanyika zaidi ya mara moja; au
v. Ikiwa kuna amri ya mahkama ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo. (kifungu cha 49, Sheria Nam. 3 ya 2018)

**3.11 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo?**

Usajili wa cheti cha kifo hufutwa kwa utaratibu ufuatao: -

i. kutolewa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo, taarifa hiyo hutolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na kupewa Muhusika wa cheti kinachotaka kufutwa;
ii. kupewa nafasi ya kujibu taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti cha kifo kwa muhusika;
iii. kufutwa kwa usajili wa cheti hicho kwa kutolewa notisi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Muhusika; na
iv. kutoa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa cheti hicho katika Gazeti Rasmi la Serikali.

**3.12 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa cheti cha kifo kukataliwa?**

Ombi la usajili wa cheti cha kifo linaweza kukataliwa endapo: -

i. taarifa za muombaji sio sahihi;
ii. ombi halikufata utaratibu uliowekwa;
iii. tukio la kifo halikutokea Zanzibar;
iv. ombi halikuambatanishwa na vielelezo muhimu vinavyohitajika;

**3.13 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa cheti cha kifo?**

Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, ndani ya Siku 30 atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri anaehusika na usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar. (kifungu cha 21(7), Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 3.14 Ni yepi Makosa katika usajili wa cheti cha kifo

Mambo yafuatayo ni makosa kufanyika wakati wa maombi ya usajili wa cheti cha kifo: -

i. kutoa taarifa za uongo;
ii. kumtumia mtu mwengine kupata cheti cha kifo;
iii. kutumia nyaraka zisizo halali;
iv. kumshawishi afisa msajili kufanya usajili kinyume na Sheria;
v. kwa uongo, kudai kupoteza au kuharibika kwa cheti ili kupatiwa cheti chengine;
vi. kurekebisha au kuingiza taarifa kwenye mfumo maalumu kinyume na Sheria;
vii. kuharibu au kujaribu kuharibu cheti cha kifo;
viii. kunyang'anya au kuchukua cheti cha mtu mwengine;
ix. kutumia cheti cha mtu mwengine;
x. kumiliki cheti zaidi ya kimoja; au
xi. kumruhusu mtu kutumia cheti cha mtu mwengine.

### 3.15 Zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu?

Adhabu za makosa yaliotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:

Faini isiyopungua shilingi za kitanzania Milioni moja na isiyozidi shilingi za kitanzania Milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili. (Kifungu cha 53(2), Sheria Nam. 3 ya 2018)

**Mfano wa cheti cha kifo**

ZANZIBAR GOVERNMENT

**Certified Copy of an entry in a Register of Deaths**

| Reg. No. | Name of Deceased | Age | Sex | Residence of Deceased | Date and Place of Birth | Cause of Death | Certified by | Name, Residence and Qualification Of Informant | Burial Permit No. and Place of Burial | Date of Registration and Signature of Registering Officer | Remarks |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | |

**Certified** to be true copy of the Entry(Reg.No.) of a Death in the Registrar of Deaths within the Town District of ……………………………………Island of Zanzibar
**FEE PAID Tsh……………** Given at the Zanzibar Civil Status Registration Agency, this…………day of …………..20………
Revenue Receipt No. ………………… of ………………….

…………………………………………………
*For* Registrar General of Births and Deaths

CENTER FOR YOUTH
DIALOGUE